IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI

N03/251/H(1)Q

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 1**

Candidate number/Numéro du candidat
Número del alumno

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |

Tuesday 4 November 2003 (morning)
Mardi 4 novembre 2003 (matin)
Martes 4 de noviembre de 2003 (mañana)

1 h 30 m

---

QUESTION AND ANSWER BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Write your candidate number in the box above.
- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all the Paper 1 questions (Text handling).
- Refer to the Text Booklet which accompanies this booklet.
- Answer the questions in the spaces provided.
- One mark is allocated per question unless otherwise indicated.

LIVRET DE QUESTIONS ET RÉPONSES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- Écrire votre numéro de candidat dans la case ci-dessus.
- Ne pas ouvrir ce livret avant d'y être autorisé.
- Ce livret contient toutes les questions de l'épreuve 1 (Lecture interactive).
- Se référer au livret de textes qui accompagne ce livret.
- Répondre à toutes les questions dans le livret de questions et réponses.
- Un point par question sauf indication contraire.

CUADERNO DE PREGUNTAS Y RESPUESTAS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- Escriba su número de alumno en la casilla de arriba.
- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todas las preguntas de la Prueba 1 (Manejo y comprensión de textos).
- Refiérase al cuaderno de textos que acompaña a este cuaderno.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.
- Cada pregunta tiene un valor de un punto, a menos que se indique algo distinto.

**KIFUNGU A — KARIBU – HOTEL YA CAPRICON**

*Soma kifungu cha habari hapa chini na kisha jibu maswali yanayofuata.*

**1.** Eleza mazingira ya Hotel ya Capricon yalivyo. *[alama 2]*

(a) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

(b) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**2.** Je ujenzi wa Hotel ya Capricon ukoje? *[alama 2]*

(a) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

(b) . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**3.** Kutokana na mazingira na ujenzi wa hoteli hiyo mahali pakoje?

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**4.** Vyumba viwili kati ya arobaini na nane vinatoa huduma zipi?

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**5.** Ni kitu gani zaidi unaweza kufanya katika mahali pa kufanyia mikutano?

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

*Chagua herufi ya jibu sahihi na uiandike katika mabano yaliyo pembeni mwa kila swali.*

**6.** Kijiji ilipo Hotel ya Capricon ni cha

A. ufugaji.
B. kilimo.
C. makumbusho.
D. mlima Kilimanjaro.

☐

**7.** Hoteli inatoa huduma gani kwenye sherehe za arusi?

A. Vitanda safi
B. Vyumba viwili kati ya hivyo ni vya ndani kwa ndani
C. Vyakula na vinywaji
D. Watu walale na kunywa

☐

**8.** Mbali na kupanda mlima Kilimanjaro, hoteli inatoa huduma gani nje ya nchi?

A. Watalii kutembelea mbuga zisizo na wanyama
B. Mbuga za Serengeti na Ngorongoro
C. Kufanya safari
D. Kusafiri ukiwa umebeba mizigo ya Kiutalii

**9.** Kutoka hotelini unaweza kutembelea mbuga zifuatazo

A. Serengeti, Ngorongoro, Ziwa Manyara.
B. Mikumi, Ziwa Victoria na Capricon.
C. Serengeti, Manyara, Ngorongoro na Capricon.
D. Capricon, Kilimanjaro, Serengeti na kwingineko.

**KIFUNGU B — CHEZA SALAMA!**

*Chagua jibu sahihi na kisha andika herufi ya jibu hilo katika mabano yaliyo katika kila swali.*

**10.** Baadhi ya sababu za kucheza michezo zimetajwa kuwa ni

A. kucheza salama huku ukiwa unafurahia na kuinua mikono juu. ☐
B. kujenga miili na akili huku ukivalia mavazi rasmi.
C. kufurahi, kupata marafiki na kusafiri.
D. kuwa mwangalifu na kuvaa mavazi ya ngoma salama.

**11.** Kigezo gani kimetumika hata mwandishi akasema kuna uwakilishi mzuri?

A. Kigezo cha kijinsia ☐
B. Mavazi ya akina kaka na akina dada
C. Kuinua mikono na wote wakafurahia mchezo
D. Wengine wana viatu wengine hawana

**12.** Ngoma imeelezwa kuwa ni nini?

A. Kifaa cha ngoma kitoacho midundo ☐
B. Kifaa cha nyimbo kiletacho furaha
C. Alama ya utamaduni wa Mwafrika
D. Ni utamaduni wa Mwafrika achezaye salama

**13.** Ni mavazi gani ambayo yanafanana kwa baadhi ya wachezaji?

A. Fulana na shanga ☐
B. Kofia na ndala
C. Kanga na Kofia
D. Kaptula na kanga

**14.** Kwa kawaida wacheza ngoma za kiutamaduni huwa wamevaa nini miguuni?

A. Ndala ☐
B. Huwa hawavai kitu
C. Viatu na soksi
D. Huvaa viatu vyeupe na soksi

**15.** Kucheza salama kumeelezwa kuwa ni nini?

A. Kutokupigana vita kwa maneno ☐
B. Kucheza bila fujo na kwa uangalifu
C. Kuheshimu mbinu za maisha bora
D. Kuvaa viatu bila kukanyagana

**16.** Kielelezo hiki kimefananishwa na nini?

A. Maisha ya wacheza ngoma za Kiafrika ☐
B. Kuingia na kutoka kwa miondoka ya ngoma
C. Kuvaa viatu na ndala miguuni
D. Mienendo na tabia katika maisha yetu

*Sentensi zifuatazo ni muhtasari wa habari uliyoisoma. Kila sentensi moja inafupisha aya moja. Chagua sentensi inayotoa muhtasari wa aya na uandike herufi yake katika nafasi iliyoachwa wazi. ANGALIA: Kuna sentensi nyingi kuliko aya zenyewe.*

***Mfano: Aya ya kwanza*** [***G***]

**17.** Aya ya pili ☐

**18.** Aya ya tatu ☐

**19.** Aya ya nne ☐

**20.** Aya ya tano ☐

**21.** Aya ya sita ☐

**SENTENSI:**

**A.** Mchezo huu ni mfano wa jinsi tupaswavyo kuishi maisha salama.

**B.** Katika mashindano haya ngoma ni kielelezo cha michezo ya vijana duniani.

**C.** Kwa mtu aliyemzoefu wa michezo atashangaa mavazi yote haya.

**D.** Wacheza ngoma hawa wana mavazi rasmi.

**E.** Wachezaji wakiwa na furaha huinua mikono juu huku wakiimba kwa sauti nene.

**F.** Kucheza salama ni kufuata kanuni za mchezo bila ghasia.

***G.*** ***Vijana wengi hupendelea michezo kwa sababu mbalimbali.***

**H.** Katika ngoma watu wote huruhusiwa hata kama hawana mavazi rasmi.

**I.** Wachezaji huwa na furaha wawapo mchezoni.

## KIFUNGU C — KUKWEPA KISWAHILI NI KUJIKANA

*Chagua sentensi kutoka sehemu B inayokamilisha sentensi ya sehemu A kama ilivyo katika kifungu cha habari. Andika herufi ya jibu lako katika mabano yaliyowekwa pembeni mwa kila swali. Angalia: Kuna sentensi nyingi zaidi katika sehemu B.*

**Sentensi Sehemu A:**

***Mfano: Mgonjwa wa akili*** [ *L* ]

**22.** Ukweli wa jambo fulani unaweza [ ]

**23.** Wanaojibadili rangi ya ngozi [ ]

**24.** Serikali kushindwa kutoa [ ]

**25.** Elimu yetu itaporomoka iwapo [ ]

**26.** Wanaotaka Kiswahili ni wale [ ]

**27.** Nchini Tanzania [ ]

**28.** Uandishi sio kazi iwezayo [ ]

**29.** Kuwa na viongozi wanaofahamu [ ]

**30.** Uandishi hulenga [ ]

**31.** Ukiitumia lugha unayoielewa [ ]

**Sentensi Sehemu B:**

**A.** kuwa ni jambo la Kiingereza na Kiswahili tu.

**B.** tutatumia Kiswahili kama lugha ya kutolea elimu.

**C.** wasiojua kitu, na wale wanaojua wanazungumza Kiingereza.

**D.** Kiingereza hakusaidii kuleta maendeleo.

**E.** kuelimisha na kuiendeleza jamii.

**F.** wanadhani kujibadili kutawafanya waoenekane wamesoma.

**G.** ionekane ina walakini katika kuamua maendeleo ya kweli yatakujaje.

**H.** bado hali ya kujisomea wenyewe ni ya hali ya chini kabisa.

**I.** unaelimika na kuwa mbunifu.

**J.** uamuzi wa tufanye nini kama Serikali kuu.

**K.** kuwa tofauti na utashi wa mtu au kundi la watu.

***L.*** ***hutilia shaka jambo ambalo kuwapo kwake ni bayana.***

**M.** kumfanya mwandishi wa Kitanzania ajitegemee kifedha.

**N.** uamuzi kuhusu lugha ya kufundishia kunafananishwa na mtu mwenye kigugumizi.

**O.** wanafananishwa na wagonjwa wa akili.

*Mwandishi ametumia dhana mbalimbali katika kutoa ujumbe wake. Sentensi zifuatazo zinafafanua dhana hizo. Tafuta dhana kutoka kwenye kifungu cha habari yenye maana sawa na sentensi zifuatazo.*

*Andika dhana hiyo katika nafasi iliyoachwa wazi katika kila sentensi.*

***Mfano: Mtu ambaye husitasita katika maongezi yake ana kigugumizi***

**32.** Kutumia Kiswahili kufundishia ni kuiua elimu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**33.** Watu wakaao sehemu moja bila kuwa na kazi maalumu . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**34.** Kiswahili ni lugha ya watu waongo wasiojua lolote . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**35.** Watu wanaokiunga mkono Kiswahili na kukitetea . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**36.** Waandishi hawawezi kutajirika kwa kuandika kwao . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**37.** Wengi wa waandishi wa Kitanzania ni fukara . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**38.** Mtu anayeipenda nchi yake na kutaka kuiendeleza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

*Kisanduku kifuatacho kina maana za msamiati uliotumika katika kifungu cha habari. Msamiati huo uko chini ya kisanduku hiki. Chagua sentensi inayoeleza maana ya msamiati na uiandike katika nafasi iliyoachwa wazi. ANGALIA: Kuna sentensi nyingi zaidi kuliko msamiatiMsamiati.*

**Msamiati**

**39.** Kuhoji ☐

**40.** Limbukeni ☐

**41.** Ina kigugumizi ☐

**42.** Kujitia kitanzi ☐

**Sentensi**

**A.** Kuning’inia huku ukivaa tai shingoni.

**B.** Kujinyonga kwa kutumia kamba.

**C.** Kuuliza uliza maswali kuhusu jambo fulani.

**D.** Mtu aliyemwenyeji na mzaliwa wa mahali fulani.

**E.** Mtu anayefikiria mara mbili kisha akasema neno na kufikiri tena.

**F.** Serikali inasitasita kutoa uamuzi kuhusu jambo fulani.

**G.** Mtu anayeanza kutumia kitu kwa mara ya kwanza.

**H.** Jambo lifanywalo ili kusheherekea tukio fulani.

**I.** Jambo linalowakutanisha watu wakacheza ngoma.

**KIFUNGU D — HADITHI – KISA CHA UADUI WA MBWA NA PAKA**

*Methali au Misemo ifuatayo imetolewa kutoka katika kifungu cha habari ulichokisoma. Kwa kila methali/Msemo andika imetoka katika Aya ipi. Aya zote zimepewa namba. Andika namba ya aya ilimotoka methali/msemo unaohusika. Methali inaweza kuwa imetoka katika aya moja au zaidi.*

***Mfano: Methali/msemo: Furaha yako ndiyo furaha yangu*** ***Aya:*** . . . . . ***3*** . . . . . .

**43.** Methali/Msemo: Penye nia pana njia Aya: . . . . . . . . . . . . .

**44.** Methali/Msemo: Urafiki wa kushibana Aya: . . . . . . . . . . . . .

**45.** Methali/Msemo: Mtegemea cha nduguye hufa masikini Aya: . . . . . . . . . . . . .

**46.** Methali/Msemo: Urafiki ni kusaidiana Aya: . . . . . . . . . . . . .

**47.** Methali/Msemo: Penye raha hapakosi karaha Aya: . . . . . . . . . . . . . . .

*Tafuta maana ya maneno yaliyokolezwa kama yalivyotumika katika habari. Chagua herufi ya jibu sahihi na uiandike katika mabano yaliyo pembeni mwa kila swali.*

**48.** **Nimekuandalieni** maana yake nini? *(Aya ya 1)* ☐

A. Nimekuandaa
B. Nimekutengeneza
C. Nimekutayarishia
D. Nimekufikiria

**49.** **Kisa** maana yake nini? *(Aya ya 4)* ☐

A. Masimulizi ya kubuni
B. Hadithi kuhusu wanyama
C. Masimulizi ya mambau zetu
D. Hadithi inayohusu mbwa na Paka

**50.** **Kujikwamua** maana yake nini? *(Aya ya 12)* ☐

A. Kujitoa katika shimo refu
B. Kujitoa katika tatizo fulani
C. Kuacha tabia ya utegemezi
D. Kujiondoa katika mawazo

**51.** **Kuhisi** maana yake ni nini? *(Aya ya 12)*

A. Kuwa na uwezo wa kutambua au kujua jambo ☐
B. Kukisia jambo kwa kunusa
C. Uwezo wa kuona mambo ya mbali
D. Kusikia kama vile kuna sauti inakuita

*Chagua neno linalofaa kujaza nafasi zilizo wazi katika kifungu hiki cha habari. Andika neno hilo katika sehemu za maswali zilizo wazi hapa chini.* ***Angalia****: Kuna maneno mengi kuliko nafasi zilizo wazi.*

*Kifungu cha habari:*

Kuwa marafiki **[ – 52 – ]** hamuwezi kutofautiana na hata kugombana. **[ – 53 – ]** sio lazima muwe maadui. Wakati mwingine marafiki hupigana lakini baadaye wakapatana. Ndiyo kawaida katika maisha. Mfano huu wa wanyama wawili Paka na Mbwa **[ – 54 – ]** maisha yetu halisi. Na mara nyingi visa, ngano au hekaya hutungwa ili sio tu kutuburudisha lakini pia kutuelemisha na kutuonya kuhusu **[ – 55 – ]** ya maisha yetu. Kwa mfano katika kisa hiki **[ – 56 – ]** mbwa anataka kujikwamua. Atokane na unyonge na dhiki aliyonayo aweze kujitegemea. Hatujaambiwa ni hatua gani lakini **[ – 57 – ]** kukisia. Walau tunaweza kusema kuwa Mbwa anataka **[ – 58 – ]** na kumtegemea paka.

*Maneno:*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| CHANDA NA PETE | ISIPOKUWA | KUONDOKANA | TUNAONA | VIONGOZI WENGI |
| HAKUMAANISHI | MIENENDO | KWA AMANI | TUNAWEZA | WAWEZAO |
| HATA KWA JAMBO | MIVUTANO | NI JAMBO | UNAAKISI | |

*Maswali:*

**52.** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**53.** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**54.** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**55.** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**56.** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**57.** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**58.** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .